optima

# MWONGOZO

KUJINUSURU NA MATUKIO YA INTANETI KUZIMWA

## Utangulizi

Mwaka 2020 nchi 29 duniani zilikuwa na matukio yasiyopungua 155 ya kuzimwa kwa intaneti. Kati ya Januari na Mei 2021, muungano wa #Keepiton uliripoti matukio 50 ambapo intaneti ilizimwa katika nchi 21 kote duniani.

**155** **MATUKIO YA KUZIMWA KWA INTANETI** Nchi 29 duniani

Utafiti uliofanywa na Shirika la Intarnews kutathmini uwezo na uwezo na changamoto zinazokabili mashirika ya uraia yanapopambana na matukio ya intaneti kuzimwa umeonesha kwamba:

> ingawa matukio haya ya intaneti kuzimwa yameongezeka duniani, watetezi (ikiwa ni pamoja na mashirika ya uraia) hawana uwezo wa kukabiliana na vitendo hivi vya intaneti kuzimwa. Isitoshe, zana za kutathmini mtandao na data husika haitumiwi na wanaharakati wanaofanya kazi katika nchi zinazoathiriwa na vitendo hivi.

Katika kuchambua matokeo na uhitaji wa kujenga uwezo wa kustahimili matukio haya miongoni mwa wananchi, mashirika ya uraia na vyombo vya habari, tumeunda mwongozo huu ili kutoa elimu muhimu kuhusu jinsi ya kukabiliana na matukio ya intaneti kuzimwa.

## 1. NINI MAANA YA INTANETI KUZIMWA?

Intaneti kuzimwa humaanisha "juhudi makusudi za kukata intaneti na mawasiliano ya mtandaoni, hivyo kuzima au kuzuia watu wasitumie huduma hii, katika eneo maalumu au ndani ya eneo fulani kwa madhumuni ya kudhibiti kuenea kwa habari."

**Kwa kawaida kuna aina tatu za kuzimwa;**

**KUZIMA INTANETI**
kuzimwa kabisa kwa intaneti ambapo huwezi kupata huduma za intaneti kabisa

**PARTIAL SHUTDOWN**
hali hii hutoke pale ambapo huwezi kufungua tovuti au mitandao fulani ya jamii

**KUPUNGUZA SPIDI YA INTANETI**
hali hii hutoke pale ambapo huwezi kufungua tovuti au mitandao fulani ya jamii

Intaneti inaweza kuzimwa katika nchi nzima au maeneo mahususi ndani ya nchi.

## 2. NANI HUZIMA INTANETI?

Vitendo vya kuzima intaneti hutekelezwa na taasisi za serikali na mashirikai yasiyo ya serikali.

**Taasisi za serikali** zinazotoa huduma za intaneti zinaweza kupewa maelekezo kutoka kwa Taasisi za usimamizi wa huduma za mawasiliano yanayowataka wazime intaneti. Kwa mfano mwaka 2021, Mamlaka ya Mawasiliano ya Uganda iliamuru makampuni ya mitandao ya simu yazime huduma za intaneti.

Mwaka 2020 iliripotiwa kwamba nchini Kenya **kundi la kigaidi la Alshabaab** lilivamia minara ya mawasiliano katika Kaunti ya Mandera na kuzima huduma za intaneti katika eneo hilo

## 3. KWA NINI WAHUSIKA HUZIMA INTANETI?

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, intaneti imezimwa kwa sababu:

**Kuzuia visa vya kuiba mtihani**
Kati ya tarehe 17-30 Juni 2021 Makampuni ya Huduma za Intaneti (ISPs) nchini Sudan yaliagizwa na Wakili wa Serikali kusitisha huduma za intaneti nchini Sudan ili kuzuia wizi wa mitihani ya kitaifa. Hatua hii ilifuata maagizo sambamba na hayo yaliyotolewa nchini Ethiopia wakati wa mitahani ya kitaifa ya mwaka 2019.

**Kudhibiti maandamano**
Serikali ya Ethiopia iliagiza huduma za intaneti zizimwe katika nchi nzima kama juhudi ya kumaliza maandamano yaliyotokea katika eneo la Oromia kufuatia kifuo cha mwanamziki maarufu Hachulu Hundessa.



**Kura za uchaguzi**
Angalu nchi 3 za Afrika Mashariki, yaani Uganda, Tanzania na Burundi zilizima intaneti wakati wa kura za uchaguzi mkuu. Serikali za nchi hizi zilizima intaneti kwa kisingizio cha kuzuia kusambaa kwa habari za upotoshaji wakati wa uchaguzi

## 4. JE, INTANETI INAPOZIMWA HUWA NA MADHARA GANI?

Kuzimwa kwa intaneti kunakiuka haki za binadamu, haki ya kupata habari na kujieleza mitandaoni. Vyombo vya habari vinakosa uwezo wa kuripoti matukio mubashara na wanahabari wanapata wakati mgumu kutafiti na kuthibitisha habari sambamba na kuwasiliana na vyanzo vya habari. Kati hali fulani, intaneti inapozimwa huathiri biashara na huduma za mtandaoni kama malipo ya simu hivyo kusababisha hasara za kiuchumi.

Intaneti inapozimwa wakati wa uchaguziwatu hukosa imani na mchakato wa kura sambamba na na kufanya kazi ya waangalizi wa uchaguzi kuwa ngumu.



**KUZIMWA KWA INTANETI KUNAKIUKA HAKI ZA BINADAMU.** HAKI YA KUPATA HABARI NA KUJIELEZA MITANDAONI

## 5. NI VIGEZO GANI HUTUMIWA KUPIMA KUZIMWA KWA INTANETI?

Intaneti inapozimwa wakati wa uchaguziwatu hukosa imani na mchakato wa kura sambamba na na kufanya kazi ya waangalizi wa uchaguzi kuwa ngumu.

### i) KIPIMO CHA OONI

Kipimo cha OONI ni programu ya kompyuta inayopatikana bila malipo iliyoundwa na Shirika la Ufuatiliaji wa Kuingiliwa kwa Mtandao yaani Open Observatory of Network Interference (OONI) ambacho kinaweza kutumiwa kutathmini viwango vya kuminywa kwa uhuru wa habari. Unaweza kupakua kipengele hiki kwenye simu yako - OONI probe mobile cha IOS au Android au kompyuta za mezani zinazotumia mfumo wa Windows, Linux na MacOS.

Kabla ya kutumia app hii ni vizuri ukumbuke kwamba kipengele cha OONI Probe sio kipengele cha kuimarisha usalama wa faragha na mtu yeyote anayefuatilia shughuli zako mtandaoni anaweza kujua kwamba unatumia kipengele cha kugundua kuminywa kwa uhuru wa habari na pili, matokeo yake yatachapishwa mtandaoni kiotomatiki.

Unaweza kutumia njia hii katika app ili ubadilishe mipangilio yako usichapishe matokeo yako. Tafadhali soma Mwongozo wa Sera ya Data wa OONI upate maelezo zaidi kuhusu data inavyokusanywa na kuchakatwa na OONI.

Mtu anapotumia kipengele cha OONI, hufanya msururu wa majaribio ili kubaini kiasi cha kuminywa kwa uhuru wa habari kwenye mitandao anayotumia. Kipengele cha OONI hupima vitu vifuatavyo:

1. **Tovuti zilizozuiliwa**
Tovuti inaweza kuzuiliwa pale ambapo juhudi makusudi zinafanywa kukuzuia kuitumia au unaelekezwa kwenye tovuti ambayo siyo au unashindwa kuingia kwenye tovuti unayotaka kutumia.

2. **Kuzuiwa kwa app za kutuma ujumbe papo hapo**
Unaweza kuangalia iwapo Mtoa Huduma zako za Intaneti (ISP) anakuzuia usitumie app za kutuma ujumbe za WhatsApp, Facebook Messenger, Telegram, na Signal.

3. **Kufungwa kwa zana za kusaidia kukwepa udhibiti wa matumizi ya mitandao**
Unaweza kuangalia kama Mtoa Huduma zako za Intaneti (ISP) anakuzuia usitumie zana mahususi (Tor, Psiphon, na RiseupVPN) ambazo zingekuwezesha kukwepa udhibiti uliowekwa

4. Uwepo wa visanduku vya katikati kwenye mtandao wako ambavyo ni ushahidi wa ufuatiliaji, kuminya matumizi ya mtandao au kuingilia trafiki ya taarifa.

5. Utendakazi wa spidi ya mtandao, na utendakazi wa kutiririsha video.

## Kutumia OONI Probe

Kwa kutumia OONI Probe, unaweza kuangalia iwapo app za mitandao ya jamii (kama vile WhatsApp na Facebook Messenger) imezuiwa kwenye mitandao yake. Ukitaka kujua kama mtandao mahususi umezuiwa, unaweza kuufanyia majaribio kupitia kitufe cha "Choose websites" kinachopatikana kwenye kadi ya Tovuti hiyo ya app OONI Probe.

Mara tu majaribio yanapokamilika, moja kwa moja utaona matokeo ya majaribio ndani ya app ya OONI Probe. Matokeo ya majaribio haya (ambayo yanajumuisha data pevu ya kipimo cha mtandao) huwa yanatumwa kiotomatiki kwa OONI na kuchapishwa mtandaoni.

*Tafadhali kumbuka kwamba ni muhimu kujua na kupitia hatari za kutumia mtandao huu kabla ya kuanza kuutumia.*

## 6. NINAWEZAJE KUFUATILIA NA KUJUA WAKATI INTANETI IMEZIMWA?



Data iliyokusanywa kwenye majaribio yote ya OONI Probe kutoka kote ulimwenguni inapatikana kupitia OONI Explorer, kanzi data kuhusu kuminywa kwa uhuru wa mtandao kote duniani. Taarifa ni muhimu sana kwa inatoa taarifa za awali katika mashauri na ripoti za matukio ya kuzimwa kwa intaneti.

### Uchambuzi wa Ugunduzi wa Kuzimwa kwa Intaneti (IODA)

IODA ni mfumo wenye dashibodi ya umma unaofuatilia intaneti mubashara ili kubaini visa vya kupotea kwa intaneti. Ni zana muhimu inayosaidia OONI kwa sababu OONI haiwezi kutumiwa katika hali ambayo hakuna intaneti kabisa. Pia kuna mashirika mengine ya kibinafsi yanayofuatilia kuzimwa kwa intaneti kama Netblocks inayochapisha taarifa za visa vya intaneti kuzimwa.

## 7. UNAWEZAJE KUJINUSURU NA MATUKIO YA INTANETI KUZIMWA?

Ikitokea unakumbwa na visa vya intaneti kuzimwa, unaweza kutumia mojawapo ya njia zifuatazo kujinusuru ili uendelee kuwasiliana kwa njia salama:

### a) Kutumia VPN. - Mfumo huu haupatikani

VPN (Virtual Private Network) huficha anwani yako ya IP na mahali ulipo na huelekeza trafiki yako kwenye seva inayomilikiwa na kampuni ya VPN, hivyo inazuiwa kuingiliwa kutoka nje k.m. Watoa Huduma za Intaneti yaani ISPs ambao wangetaka kuingia au kuizuia. Kwa sababu mtoa huduma za VPN anaweza hata hivyo kuona data zako za kibinafsi, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha unachagua mtoa huduma za VPN anayeaminika.



Unapotafuta mtoa huduma za VPN anayeaminika, chagua inayofikika kiurahisi, ina code iliyochapishwa mtandaoni na iliyotathminiwa na mtaalamu wa usalama wa mtandaoni anayeaminika. Kwa bahati mbaya, matumizi ya VPN yanaweza kusababisha kasi ndogo ya intaneti na wakati mwingine VPN inaweza kuzuiwa ikiwa kuna kufungwa kwa intaneti kwa muda. Ili kujinusuru na hali hii, huenda ukalazimika kutumia seva ya nje iliyoko nje ya nchi kwa sababu mamlaka za nchi unakotumia mtandao hawaijui na hawawezi kuifunga.

Unahimizwa kutumia VPN katika hali ambazo intaneti imezimwa kwenye tovuti fulani ambaoo majukwaa fulani hayapatikani. Kitu muhimu cha kuzingatia unapochagua VPN ni usalama wako. Zingatia yafuatayo:

# KITU MUHIMU CHA KUZINGATIA UNAPOCHAGUA VPN

01 Nchi ambako huduma hiyo ya VPN imesajiliwa na mahali ambako seva zao zinapatikana kwa sababu zinasimamiwa na sheria na watatakiwa kutekeleza maelekezo kutoka kwa serikali na mamlaka za utekelezaji kuhusu data.

02 Hungependa kujulikana unapotumia VPN

03 Ikiwa VPN zimepigwa marfuku au zimeharamishwa katika nchi yako

04 Tafadhali kumbuka kwamba VPN haibani taarifa zako muda wote na huenda ukalazimika kutumia zana nyingine za kuzuia kujulikana.

05 Data unayoweka na muda inaohifadhiwa

### B) KUPERUZI SALAMA

Muda ambao intaneti imezimwa ni muhimu kuperuzi kwenye tovuti salama zinazotumia protokali ya HTTPS kwa sababu sio rahisi kuingiliwa na husimba shughuli zako mtandaoni kwa njia fiche. Kifupi ni kwamba, kutumia tovuti salama kunasaidia kuzuia wadakuzi wa mitandao kuona au kufuatilia shughuli zako mtandaoni. Hii ni muhimu hasa pale ambapo Serikali au vyombo vya usalama wanafuatilia kile wananchi wachoperuzi wakati intaneti imezimwa.

Unaweza kuweka mipangilio ya HTTPS Everywhere, kipengele kinachoongezwa kwenye kivinjari chako kinachokuruhusu kuperuzi kwa usalama kwenye tovuti salama au kwenye sehemu salama za tovuti.

Ni muhimu kusistiza kwamba kipengeke cha HTTPS Everywhere hulinda maudhui unayoperuzi na hakifichi utambulisho wa tovuti unazotembelea wala muda unaotumia kwenye tovuti hizo. Makala haya yanatoa maelezo kuhusu jinsi ya kuweka mipangilio ya kipengele cha HTTPS Everywhere kwenye kivinjari chako, ulinzi unaopatikana kwa kuweka kipengele hiki, data inayokusanywa na jinsi ya kuiondoa.

### c) Kuweka TOR Browser

Tor ni programu inayosaidia watu kivinjari kwa fargha na bila kujulikana kwa kuzuia wadakuzi kujua tovuti unazotembelea sambamba na mahali ulipo, hatua inayosaidia kipengele cha HTTPS Everywhere. Mara nyingi hutumika kwenye Kivinjari cha Tor kinachoweza kuwekwa kwenye Windows, linux na android. Kwenye kivinjari cha Tor, historia yako ya kuvinjari hufutwa mara tu unapomaliza kuperuzi.

Kadri intaneti inavyozimwa zaidi, ndivyo inavyokuwa vigumu kukwepa athari za kuzima intaneti kwa hiyo tunakushauri uweke zana hizi mapema.

## 8.KUTETEA DHIDI YA KUZIMA MTANDAO

Utetezi huleta ufahamu wa madhara yanayosababishwa na kuzimwa kwa intaneti na inaweza kusaidia katika kulinda haki za watu kupitia kushiriki maelezo kuhusu jinsi ya kushughulikia kuzima kwa mtandao na kuangazia zaidi hatua ambazo watu wanaweza kuchukua ili kujiandaa kwa kuzima kwa mtandao.

Ingawa inaweza kuwa vigumu kubuni kampeni ya kutosha ya utetezi, kwa kuwa hakuna mbinu ya "ukubwa mmoja unaofaa wote", nyenzo zifuatazo za utetezi hutoa mwongozo na mifano ili kusaidia juhudi za utetezi wa kuzimwa kwa mtandao na kujumuisha mwongozo na mifano ya kukusaidia katika kujenga ujumbe wenye matokeo. na kupata neno hata wakati wa shida.

Maktaba ya rasilimali ya OPTIMA inajumuisha orodha ya kukaguliwa kabla ya kuzima ambayo inaeleza hatua ambazo watu wanaweza kuchukua katika kutayarisha kukatizwa kwa mtandao kabla ya uchaguzi na njia mbalimbali za kukwepa kuzima kwa mtandao.

## 9. JINSI YA KUKABILIANA NA KUKATIKA KWA MTANDAO MAHAKAMANI

Wakati fulani, mahakama inaweza kuwa njia bora zaidi ya kuzuia kufungwa na inapofikia hatua hii ya kutatua kuzimwa kwa mtandao. Ni vyema kuwa na ufahamu mzuri wa masuala husika, sheria, viwango vya kisheria na sheria linapokuja suala la kuzimwa kwa mtandao. Kisha hii inatumika katika mashauri ya kimkakati kupitia mahakama ili kupinga na/au kuzuia kufungwa huku kukizingatiwa haki za binadamu mtandaoni.

Katika kuandaa kupinga kuzima kwa mtandao mahakamani, Ni muhimu kuandika na kuhifadhi shughuli zinazotokea. Kwa mfano, data kutoka kwa majaribio ya uchunguzi wa OONI inaweza kutumika kama ushahidi wa shughuli kama hizo na ushahidi wowote wa video unaoonyesha kuzima. Ili kujifunza zaidi kuhusu njia mbalimbali za kuzima hati, soma mwongozo huu.

Maktaba ya OPTIMA Inajumuisha nyenzo za kukusaidia kujenga na kubishana katika kesi kali na kujifunza kuhusu changamoto za kisheria zilizofanikiwa kutoka kote ulimwenguni ili kufahamisha mipango hiyo.

## 10.JE, NINAWEZA KUPATA WAPI MAELEZO ZAIDI AU NYENZO KUHUSU KUZIMA KWA MTANDAO?

Maktaba ya rasilimali ya OPTIMA ni zana iliyotengenezwa ili kutoa taarifa kuhusu jinsi ya kushugulikia kuzimwa kwa mtandao.

Ni mkusanyiko wa rasilimali mpya na zilizopo, miongozo, mbinu na zaidi ili kusaidia watu binafsi na wanaharakati kabla, wakati na baada ya kuzima kwa mtandao.
Ili kujifunza zaidi kuhusu nyenzo hii, tembelea https://preparepreventresist.org/

Fuatilia shughuli za mashirika mbalimbali ya kiraia chini ya muungano wa #Keepiton unaofanya kazi kupambana na kuzimwa kwa intaneti kote ulimwenguni.